



Fisi- maji mkubwa wa Afrika (*Aonyx capensis*) Karibia kutishiwa kutoweka (IUCN Red List)



Nyaya ni 60-90mm upana. Unyayo wa dume ni mkubwa kuliko wa jike



Fisi-maji mkubwa wa Afrika ni mkubwa; kichwa na mwili inafikia urefu wa mita moja (1m), mkia 50cm na uzito wake huwa 10-20kg. Sehemu ya juu ya mwili wake una rangi nyeusi ambayo haijakolea, kidevu, mashavu, koromeo na kifua kote kweupe. Masharubu marefu sana, mengi na ya rangi nyeupe. Yanamsaidia katika kutafuta chakula chake kikuu ambacho ni kaa ambao hukamatwa kwa mikono yake mahiri isiyokuwa na kucha. Katika mazingira ya maji baridi, mara nyingi hula kaa wa majini na kwa kiasi kidogo vyura, samaki, na kwa musimu wadudu aina ya Kereng`ende wadogo (dragon fly larvae)

Fisi-maji kujikausha maji na kujikuna kwa kugaragara kwenye nyasi au kwenye mchanga pembezoni mwa kingo za mto, au miamba ya mawe. Katika maeneo mengi ambayo hutumika kwa kujigaragaza, sehemu za kurundika choo hutambulika na kutumika mara kwa mara kama ilivyo kwa sehemu ya kugaragara. Wakati anajisaidia fisi-maji huwa anazunguka huku akiendelea, na kinyesi chake hudondoshwa kumzunguka kikiwa kimevunjikavunjika katika vipande vifupi, na ncha zake hazijabondeka kote. Kinyesi kibichi huwa na rangi nyeusi ambayo hajiakolea, hubadilika na kuonekana kuwa na rangi ya maziwa wakati kimekauka, kawaida hufikia mduara wa 25mm, makadirio ya 22-30mm.



Kinyesi kibichi mduara wa 20-32mm kawaida Zaidi ni mabaki ya kaa, yawezekana pia samaki. Hakuna mbevu, nywele.



Kinyesi cha fisi-maji - kibichi (kushoto); cha zamani (chini)



Kinyesi cha fisi-maji na Nguchiro-maji vinachanganya. (Kulia) kinyesi cha Nguchiro-maji ni kidogo kiasi mduara wa 15-22mm na kina mabaki ya kaa, wanyama wadogowadogo (nywele) wadudu jamii ya panzi, mayoya ya ndege.

Kinyesi cha Nguchiro-maji



Watu wa Mtanndao unaojikusisha na uhifadhi wa Fisi-maji wa Afrika wanatafuta taarifa za sasa kuhusu mtawanyiko wa Fisi-maji. Kama wameonekana, tafadhali toa taarifa kupitia, africanotternetwork@gmail.com Wapi, lini, wangapi wameonekana na taarifa nyingine zote kuhusiana na kuonekana kwao. Picha zinakaribishwa sana!